

Biblia inasemaje....

“Yesu aliachukuliaje maandiko”

Sehemu ya pili

“Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki.” 2 Timotheo 3:16.

“Daudi mwenyewe alisema, kwa uweza wa Roho Mtakatifu,” Marko 12:36.

Katika Marko 12:35-37, Yesu alikuwa akiwathibitishia viongozi wa masinagogi na watu wengine kwamba alikuwako kabla ya Daudi, na kwana ndiye Bwana wa Daudi na kwa hiyo ni wa milele. Watu wa kawaida walifurahia kusikia ujumbe wake. Walakin maadui wa Yesu walifura hasira kutohana na mafundisho yake. Katika sehemu Yesu alitumia maneno ya Daudi yaliyoko katika Zaburi 110:1 akisema kuwa ni ya Roho Mtakatifu. Maana ya Yesu hapa ilikuwa ni kwamba Daudi hakuandika maneno yale kama apendavyo yeye tu ama kwa njozi. Ni Roho Mtakatifu aliyeleta ukweli ule utokao kwa Baba.

Kwa hiyo, Yesu anatufundisha leo kuwa maandiko hata tangu Agano la Kale yana pumzi ya Mungu! Katika Mathayo 24, Yesu akaanza kuongelea ujio wa kuteketetea kwa Yerusalem. Katika Mathayo 24:15 , Yesu akasema;

“Hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililotabiriwa na nabii Daniel, limesimama katika Patakatifu,” Hapa sasa Yesu alikuwa anazungumzia ujumbe wa kinabii uliotolewa na Daniel amabao uliandikwa miaka 550 kabla, Daniel 9:23,25,27 na 12:1. Naye Yesu aliongelea unabii uliomo katika aya hizi za unabii kwamba ni kweli, na kuwa unabii huu usingetanguka na ungetimia.

Pasina shaka kabisa, kitabu chochote kizuri kilichoandikwa kuhusu historia ya Israel katika karne ya kwanza kitaeleza kuhusu jinsi Mji wa Daudi-Yerusalem ulivyoteketea kikamilifu. Yesu alijua kuwa maneno aliyoadika

Daniel yalivuviwa na kwamba yanetimia punde. Na yakinmia mnanmo 70 A.D.

Yesu akiwa ameenenda huku ametuacha nyayo ili tuzifuate, alituachia nyayo zinazofundisha kuwa alisadiki kuwa maandiko ni pumzi ya Mungu. Alisadiki kuwa maneno ya Mungu yamevuvuviwa na kuwa Roho Mtakatifu aliratibu uwiano wa maandiko.

Vipi kuhusu wewe, unasadiki?